**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, WAKATI WA KUFUNGUA MKUTANO WA KWANZA WA KITAIFA WA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050+, DODOMA, TAREHE 9 DISEMBA, 2023**

- *Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Tanzania;*
- *Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar;*
- *Mheshimiwa Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*
- *Komredi Abdulrahman Kinana, Makamu Mwenyekiti wa CCM (Bara);*
- *Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*
- *Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*
- *Mheshimiwa Anna Makinda, Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*
- *Mheshimiwa Job Ndugai, Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*
- *Bw. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mwakilishi wa Mheshimiwa Jaji Mkuu;*
- *Waheshimiwa Wanasheria Wakuu wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa SMZ;*
- *Mhe. Prof. Kitila Mkumbo(Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji;*
- *Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wa SMZ;*
- *Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

- *Mhandisi Zena Said, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa SMZ;*
- *Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji na Makatibu Wakuu na Viongozi wengine wa Serikali mliopo;*
- *Wakuu wa Taasisi mbalimbali mliopo;*
- *Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;*
- *Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wote wakiongozwa na Mhe. Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;*
- *Waheshimiwa Wabunge;*
- *Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya wote mliopo;*
- *Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma na Mameya wengine wote mliopo, pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri, Miji na Majiji;*
- *Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Taasisi za Kimataifa;*
- *Ndugu Lawrence Mafuru, Katibu Mtendaji, Tume ya Mipango;*
- *Profesa Lucian Msambichaka, Kiongozi wa Kamati ya Kitaifa ya Dira na Wanakamati wote;*
- *Dkt. Maryam Vuai, Kiongozi wa Timu ya Kitaluma ya Dira;*
- *Viongozi wa Vyama vya Siasa mliopo;*
- *Viongozi wetu wa Dini na Viongozi wa kimila (Machifu);*
- *Watumishi mbalimbali wa Serikali mliopo;*
- *Wawakilishi wa Wadau wa Maendeleo, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia;*
- *Wananchi wote mnaofuatilia tukio hili kwenye Vyombo vya Habari;*
- *Ndugu Wanahabari, Vikundi vya Burudani;*
- *Wanafunzi mliopo nasi;*
- *Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;*

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**Umoja na Mshikamano!. Ni chachu ya Maendeleo ya Taifa**

***Ndugu Wananchi,*** Niungane na walionitangulia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na kutuwezesha kuhudhuria Mkutano huu wa Kwanza wa Kitaifa wa Dira ya Taifa ya Maendeleo. Shughuli hii ni muhimu sana na kwa umahsusi wake tumeamua kuifanya leo tukiwa tunaaadhimisha miaka 62 ya Uhuru.

**SALAAM ZA POLE NA MAOMBI**

Kabla sijaendelea na mukhtadha wa shughuli hii, niruhusuni niwaombe tusimame kwa ajili ya kutoa heshima kwa Watanzania wenzetu waliopoteza maisha huko Katesh, Wilaya ya Hanang, Mkoa wa Manyara kufuatia mafuriko yaliyotokea tarehe 2 Disemba, 2023. Mwenyezi Mungu apumzishe roho zao mahali pema peponi. Amina. Aidha, tuwaombee, majeruhi wetu wapate uponyaji wa haraka.

Ndugu zangu, katika mnasaba wa shughuli yetu ya leo, nitumie fursa hii pia kuwaombea viongozi wetu wote wa kitaifa waliotangulia mbele ya haki hususan wale waliopigania na kuuendeleza uhuru wetu.

**UTANGULIZI**

Sasa, kwa dhati kabisa, namshukuru Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri, pamoja na Mtendaji Mkuu, Wataalamu na Watumishi wa Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) na wale wa Tume ya Mipango kwa maandalizi mazuri yaliyofanikisha Mkutano huu.

**SALAAM ZA HERI KWA SIKU YA UHURU**

Leo tarehe 9 Disemba mwaka huu tunaadhimisha miaka 62 ya Uhuru wa Tanganyika kwa sasa Tanzania Bara. Hivyo, nitumie fursa hii kuwatakia kheri

katika maadhimisho haya. Katika ujenzi wa taifa miaka hii inatosha kabisa kufanya tathmini ya mapito yetu na kubainisha njia muafaka za kutusogeza mbele zaidi; kwani, muda huu umetupa uzoefu na ukomavu wa kujiendesha na kujisimamia. Hivyo, tunayo kila sababu ya kujipongeza kwa kuwa tumeweza kujenga umoja wa kitaifa na kupiga hatua kubwa za kimaendeleo. Licha ya changamoto mbalimbali tulizopitia, kwa ujumla, miaka 62 ya Uhuru wetu imekuwa ni ya mafanikio kwa kiasi kikubwa. Pamoja na amani na utulivu, nchi yetu imepata maendeleo makubwa kwenye kila sekta, iwe za kijamii au za kiuchumi.

***Ndugu Wananchi,*** Ujenzi wa nchi, ni suala endelevu, au kwa lugha ya siku hizi, ni mchakato. Hivyo, katika kila awamu ya uongozi wa nchi yetu kuna mchango wa maendeleo ya nchi yaliyofanyika. Mafanikio tuliyonayo leo, ni matokeo ya uongozi thabiti, maono na michango wa viongozi walionitangulia. Nitumie fursa hii, kuwashukuru na kuwapongeza sana viongozi hao, ambao ni Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mzee Ali Hassan Mwinyi, Hayati Benjamin William Mkapa, Mzee Jakaya Mrisho Kikwete na Hayati John Pombe Magufuli, pamoja na wasaidizi wao wote, ambao wengine tunao leo hapa. Maono na ushupavu mkubwa katika uongozi wao, ndio matunda tunayoyafaidi leo hii. Ahadi yangu ni kuyaendeleza mema yote yaliyoiletea nchi yetu maendeleo na kujifunza kutokana na changamoto walizokutana nazo.

Pamoja na uongozi thabiti, nguzo nyingine muhimu iliyotufikisha hapa ni amani, umoja na mshikamano wetu. Ndio maana, Kauli mbiu ya maadhimisho yetu ya mwaka huu inasema ***"umoja na mshikamano ni chachu ya maendeleo ya Taifa letu".*** Tunapotakiana kheri kwa kuadhimisha miaka 62 ya Uhuru, rai yangu kwenu, ni kuwasihi tuendelee kudumisha umoja na mshikamano wetu ili tuweze kufanya kazi kwa bidii, ubunifu na maarifa zaidi, katika jitihada za kustawisha jamii ya Watanzania na kuimarisha Taifa kwa ujumla.

**TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA DIRA YA 2025**

**Ndugu zangu**, waswahili wanasema ***"usipojipangia, utapangiwa"***. Sasa kupangiwa kuna hasara zake, anayekupangia, ndio anaweka faida zake kwenye mipango anayokupa**.** Lakini ukijipangia, unapanga wewe mwenyewe kwa faida yako mwenyewe. Nyenzo mojawapo iliyotuwezesha kufikia tulipo ni Dira ya Maendeleo ya Taifa.

Pengine mtajiuliza na wale wanaotufuatilia kwenye vyombo vya habari, watajiuliza, dira ni nini na umuhimu wake ni upi kwa nchi? Nikitumia mfano rahisi, Dira ni chombo kinachotumiwa na nahodha wa meli inayomuelekeza njia ya kufikia anakolenga kwenda, na kumonesha yale yote yaliyoko njiani, ili aepukane nayo na aweze kufika anakokwenda. Vivyo hivyo, Dira ya Maendeleo, ni andiko maalum linaloainisha mipango iliyowekwa, mikakati itakayotekelezwa na rasilimali zitakazotumika katika kipindi kitakachowekwa ili kufikia malengo yanayokusudiwa ya maendeleo ya Watu na Taifa kwa ujumla. Kwa kawaida Dira hutafsiriwa katika mipango midogo ya maendeleo kwa urahisi wa utekelezaji.

Ili kuwa na mipango shirikishi, iliyochangiwa mawazo na wadau wengi nchini, uandaaji wa Dira ya maendeleo hushirikisha makundi mbalimbali ya Wananchi na wadau wa maendeleo. Kwa lugha nyingine, Dira ya Taifa ni namna ya kisayansi ya kukubaliana kuhusu aina ya maendeleo, kasi ya utekelezaji wake na rasilimali zitakazotumika. Hili ndilo tunalolizindua leo.

***Chimbuko la Dira ya mwaka 2025***

***Ndugu Wananchi,*** Miaka ya 1980 na 1990 nchi yetu ilipita katika kipindi kigumu cha kiuchumi kilichochangiwa na mazingira ya kiuchumi ya kimataifa. Taifa letu lilikabiliwa na kiwango kisichoridhisha cha ukuaji wa uchumi, uhaba mkubwa wa bidhaa na huduma muhimu, mfumuko mkubwa wa bei, upungufu

wa mapato yatokanayo na mauzo nje, madeni makubwa na yasiyohimilika, na makusanyo madogo ya mapato ya ndani ya Serikali. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali ilichukua hatua kadhaa za maboresho na kupanga mipango ya maendeleo itakayokuza uchumi wetu. Hilo ndilo lilikuwa chimbuko la Dira ya Maendeleo ya Taifa ya miaka 25 (mwaka 2000 hadi mwaka 2025), iliyozinduliwa mwaka 1999. Baada ya Dira hiyo kuzinduliwa, maboresho mbalimbali ya kisera, kitaasisi na kimfumo yalifuata kuanzia miaka ya 2000.

Wakati Dira inazinduliwa, nchi yetu ilikuwa ikikabiliwa na mzigo mkubwa wa deni la nje. Tulilazimika kuingia kwenye Mpango wa Unafuu wa Madeni wa taasisi za kifedha za kimataifa (Multilateral Debt Relief Initiative - MDRI) na Mpango wa Kusamehe Madeni ya Nchi Maskini Sana (Highly Indebted Poor Countries Initiative - HIPC). Hivyo, Serikali ililazimika kuandaa mipango ya muda wa kati katika mfumo wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini (Poverty Reduction Strategy Paper - PRSP), hapa ndipo kukawa na ile Mikakati ya Kupunguza Umaskini iliyojulikana kama MKUKUTA.

Mnamo Mwaka 2009/10 ilifanyika tathmini ya utekelezaji wa malengo ya Dira, ambapo Serikali ikaja na Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (Long-Term Perspective Plan - LTPP) 2011/12 – 2025/26 uliogawanywa katika vipindi vitatu vya miaka mitano-mitano. Kwa sasa tuko kwenye kipindi cha miaka mitano ya mwisho ya utekelezaji wa Mpango huo Elekezi ambao tutaumaliza mwaka 2025.

Ndugu zangu, katika Mkusanyiko huu, tumeshuhudia Taifa ikipokea taarifa ya kitafiti ya tathmini ya utekelezaji wa Dira ya 2000/ 2025. Tathmini hiyo, kama ilivyoelezwa na Pfof. Kitila Mkumbo kwa kifupi, itachangia katika kuandaa Dira mpya ya Maendeleo kwa kipindi cha miaka 25 ijayo. Niwapongeze sana wataalam wa Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Jamii (ESRF) wakiongozwa na Profesa Fortunata Makene kwa kazi hii kubwa waliyoifanya. Niwashukuru pia wataalam na wadau wote ambao walichangia zoezi hili la tathmini.

Kama mlivyosikia, Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2000/25 ilijengwa juu ya nguzo kuu nne ambazo ni: kuboresha hali ya maisha ya Watanzania; kuwepo kwa mazingira ya amani, utulivu na umoja; kujenga utawala bora na utawala wa sheria; na kujenga uchumi imara unaoweza kuhimili ushindani kutoka nchi nyingine au mataifa mengine. Kutokana na nguzo hizo, Dira iliweka viashiria vya kupima utekelezaji wa kila lengo. Na utekelezaji wake, ni kama ulivyowasilishwa na Prof. Kitila Mkumbo. Hapa mimi nitagusia maeneo machache halafu niende kwenye mapendekezo yangu.

***Usalama wa Chakula***

Kwa upande wa sekta ya kilimo, ni ukweli kwamba nchi yetu imefanya kazi nzuri sana. Kwa sasa Tanzania inajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 124 tukielekea utoshelevu wa asilimia 140% ifikapo mwaka 2025. Suala lililo mbele yetu ni lishe na usalama wa chakula chenyewe.

Sasa pamoja na kuwapongeza wote waliofanya kazi hii ndani na nje ya Serikali, ni lazima Dira mpya itilie maanani ukweli kwamba dunia inakabiliwa na uhaba na kutokuwa na usalama wa chakula. Matarajio ya Dira inayoandikwa ni kuweka lengo la kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji wa chakula kwa ajili ya Bara la Afrika na kwengineko duniani.

***Elimu***

Kwa upande wa elimu, Dira ilitutaka tuhakikishe kwamba watoto wote wa Tanzania wanapata elimu ya msingi na wafike hadi darasa la saba. Lakini pamoja na takwimu zilizoelezwa na Prof. Kitila Mkumbo, leo hii tunapoongea tumekamilisha lengo hilo, na sio tu kwamba watoto kufika darasa la saba, lakini tumesema watoto waende mpaka kidato cha nne na bila kulipa ada yeyote. Kwa hiyo hapa napo tumefanya vizuri.

Licha ya ongezeko na kuimarika kwa miundombinu ya elimu na wahitimu, bado kuna haja ya kuongeza hadhi ya elimu inayotolewa. Hivyo, Dira mpya, ni lazima ielekeze kujibu maswali yanayohusu elimu yetu na mchango wake katika maendeleo ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Takwimu mbalimbali zilizooneshwa hapa ni takwimu zinazoishia mwaka 2022. Mipango yetu na malengo yetu yanakwenda mpaka 2025. Tunaelewa kwamba kwa sasa nchini kote kuna miradi mbalimbali, ya maji, umeme, na barabara. Ni imani yetu kwamba tutakapofika mwaka 2025, yale malengo tuliyowekewa na Dira tunakwenda kuyakamilisha yote.

***Amani, utulivu na umoja***

Kwenye suala la amani, utulivu na umoja, kama ilivyosemwa hapa, kwamba, sote tunashuhudia kutekelezwa kwa lengo la kudumisha amani, utulivu na umoja. Nchi yetu imeendelea kuwa na amani na utulivu kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Dira ya 2000/25. Ninawasihi tuendelee kudumisha tunu hii kwa mustakabali mwema wa Taifa letu.

Ili kukuza mshikamano wa Kitaifa, Serikali itaendelea kutekeleza Falsafa yake ya R nne (4Rs) ambayo pamoja na mambo mengine, inasisitiza kuwa, maridhiano pamoja na kujenga masikilizano katika jamii yetu kutatuwezesha kupanga na kutekeleza vyema mipango yetu ya maendeleo na kukubaliana katika kuleta mabadiliko na kuimarisha Taifa letu kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Dira nayo iende kuangalia na hii. Dira tunaimalizia imetuagiza kuweka utulivu, usalama na amani. Lakini Dira tunayokwenda kuandika tutakwenda hatua mbele zaidi katika kutekeleza hayo.

***Utawala bora na utawala wa sheria***

Kwa upande wa utawala bora, maendeleo yaliyopatikana ni kutokana na uwepo wa Utawala Bora na Utawala wa Sheria, licha ya changamoto zilizopo;

tunakiri zipo. Kama mnavyofahamu Mwezi Januari, 2023 Serikali iliunda Tume ya kuangalia jinsi ya kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini ikiwa ni namna ya kuendelea kuangalia njia nyengine bora zaidi za kudumisha utawala bora na utawala wa sheria nchini.

Ni imani yangu kuwa, Dira mpya itanufaika na mapendekezo yaliyotolewa na Tume hiyo, ili tuendelee kuimarisha zaidi mifumo ya haki jinai nchini na hivyo kudumisha utawala bora na utawala wa sheria.

***Mchango kwenye mjadala kuhusu Dira inayoandaliwa***

***Ndugu Wananchi,*** nilipata bahati ya kuipitia tathmini, na baada ya kuipitia tathmini ya utekelezaji wa Dira ya 2000/25, nimeona kuna mambo ambayo yanapaswa kuyatazama zaidi wakati tunakamilisha utekelezaji wa Dira hii ifikapo mwaka 2025 na tunapoandaa Dira mpya.

Maeneo ambayo yanapaswa kuangaliwa na kupewa kipaumbele katika Dira mpya ni kama ifuatavyo:

**Kwanza,** ukuaji wa uchumi kufungamanishwa na sekta za uzalishaji kama sekta za kilimo na sekta nyingine za uzalishaji, ambapo sekta ya kilimo kwa sasa inakuwa kwa asilimia 4 lakini lengo letu ni kuendelea kuikuza zaidi. Ni lazima mipango yote ifungamanishwe na sekta hiyo.

**Pili**, ni kupata takwimu kutoka sekta isiyo rasmi. Inawezekana kabisa katika eneo la kukuza uchumi tumefanya kazi kubwa na uchumi umekua kwa kiasi kikukbwa, lakini kwa sababu hatuna takwimu za sekta isiyo rasmi, tumejikita kwenye sekta iliyo rasmi. Hivyo tuangalie jinsi ya kuwa na mfumo utakaoshirikisha sekta isiyo rasmi ili tuweze kupata takwimu zake.

Kwenye kigezo cha kuongeza pato la wananchi, inaendana na hili (la takwimu kutoka sekta isiyo rasmi). Inawezekana tumefanya vizuri zaidi, na

tunakaribia lile lengo tulilowekewa. Lakini kwa sababu hatuna taarifa za sekta isiyo rasmi, tumejikita kwenye taarifa zetu tu.

Hivyo tunavyoanza zoezi la kuandaa Dira mpya hatuna budi kufikiria ni kwa namna gani tutachochea ukuaji wa uchumi kwenye maeneo ya uzalishaji, yanayowagusa wananchi wengi zaidi na yanayotengeneza ajira kwa ajili yao.

Eneo la **Tatu** ni suala la tathmini na ufuatiliaji (*monitoring and evaluation*), ambalo kwa kiasi kikubwa huko nyuma hatukulipa umuhimu mkubwa. Kwenye Dira tuliagizwa kufanya tathmini na ufuatiliaji, lakini tumefanya mara moja tu katikati ya utekelezaji wa Dira yetu (mid-term review). Inawezekana tungefanya tathmini kila baada ya muda tungebaini viashiria mapema, tungerekebisha na tungekwenda vizuri zaidi.

Uwepo wa taasisi ya Tume ya Mipango itakwenda kuondosha kasoro hiyo na kuhuisha suala la tathmini na ufuatiliaji si katika utekelezaji wa Dira ijayo tu, bali katika utekelezaji wa mipango yote ya maendeleo ya nchi yetu.

**Nne,** Eneo lingine linalohitaji kufanyiwa maboresho zaidi ni uratibu wa kufungamanisha miradi na vipaumbele kwa sekta zinazohusika katika uzalishaji, suala ambalo limetufanya tupate manufaa kidogo kuliko ambavyo tungeweza kupata.

Kwa mfano, tunapozungumza kutoa maji Ziwa Victoria kuja Dodoma, kwa muda mrefu tumejielekeza kuleta maji safi na salama kwa ajili ya matumizi. Lakini kumbe tungeutumia mradi huohuo kwa kuongeza kilimo cha umwagiliaji huko ambapo maji hayo yanapita. Ndio ufungamanishaji ninaouzungumzia.

Katika hili, Matarajio ni kwamba, Kamati ya uratibu wa uandaaji wa Dira mpya italenga kuhakikisha kuwa tunapotekeleza mipango inayotokana na Dira mpya kwenye sekta moja, inakuwa na mwingiliano na mchango katika

kuboresha sekta nyingine. Ni kwa namna hii tu ndipo tutatumia rasilimali zetu chache ipasavyo na kwa njia nzuri zaidi.

Eneo la **Tano** ni mchango mdogo wa mashirika ya umma katika kukuza uchumi wa nchi. Mbali na hatua zilizoanza kuchukuliwa kupitia Msajili wa Hazina, Dira iweke mwelekeo wa Uwekezaji na usimamizi wa maboresho ya kiutendaji wa Mashirika ya Serikali ili yaongeze ufanisi katika uendeshaji na yaweze kuhimili ushindani wa kikanda na kimataifa.

Eneo la **Sita** ni ushiriki wa sekta binafsi ya ndani na kutoka nje ya nchi. Kwa upande wa Sekta binafsi ya ndani, ni lazima iendelee kuimarishwa na iwe tayari kuimarika. Ili sekta za uzalishaji ziwajibike vyema taasisi za sekta binafsi za wenyeji zinatakiwa kuwa na uwezo na utayari wa kupokea na kushirikiana na wageni wanaokuja kuwekeza nchini, kufanya biashara, na kutengeneza ajira kwa wananchi, na hatimaye, kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi wetu.

Hivyo, ni matazamio yangu kwamba mtaangalia pia nafasi ya Mashirika ya Umma na taasisi za Sekta Binafsi katika kufikia malengo ya Dira mpya tunayoiandaa.

**(Saba)** Tathmini inatuonesha kuwa tumepiga hatua katika kuweka mifumo ya kuongeza uwazi na kusimamia maadili kwenye utumishi wa umma. Hili tutaendelea kulisimamia. Lakini jamii yetu ni zaidi ya utumishi wa umma; sehemu kubwa zaidi ya jamii yetu ipo nje ya utumishi wa umma. Huko hakuna mifumo ya moja kwa moja ya kusimamia maadili.

Kama nchi lazima tuwe na misingi inayotuongoza na tunayoizingatia kwa uzito mkubwa. Lazima tuwe na jamii yenye ujasiri wa kuhoji wanaojipatia mali wasizo na maelezo nazo, jamii inayochukia rushwa kila mahali, jamii inayoweza kujituma na kufanyakazi bila kusukumwa, jamii inayopinga uchakachuaji wa mazao kama pamba na korosho kuongezwa mawe, jamii

inayolaani ukwepaji kodi, jamii ambayo haiwaibii waathirika wa ajali badala ya kuwaokoa.

**Tuamue kujenga jamii ya watu mahiri, makini na waadilifu. Jamii yenye maadili.** Sina shaka kwamba suala hili litapewa uzito mkubwa kwenye mjadala wa kuandaa Dira mpya na pia kuangalia ni kwa namna gani Serikali na taasisi zisizo za kiserikali ikiwemo taasisi za kidini zitakavyochangia kujenga maadili yetu.

Misingi hii, sio tu itajenga jamii bora bali pia itawavutia wengi zaidi kuja Tanzania na kutufungulia fursa zaidi na zaidi. Tunapoandika Dira mpya, lazima tuone uwezekano wa kuwa na Maadili ya Taifa.

Eneo la **Nane** ni kubaini viashiria hatarishi na kuviwekea udhibiti. Uzoefu tulioupata katika utekelezaji wa Dira ya mwaka 2025 ni kwamba, kumekuwa na matukio makubwa ya kimazingira kama *El Nino*, ukame na uvamizi wa wadudu waharibifu, Matukio ya maradhi kama *Cholera* (kipindupindu) au UVIKO 19, kuharibika kwa usalama wa Dunia (Vita vya Kikanda vinavoendelea) ambayo yamekuwa nje ya uwezo wetu kuyadhibiti au uwezo mdogo wa kukabiliana nayo. Mambo haya yakitokea yanaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Mathalan, mvua kubwa za *El Nino* za mwaka 1998 zilizoharibu miundombinu katika sehemu kubwa na nchi yetu na kufuatiwa na ukame mkubwa sana uliosababisha uhaba mkubwa wa chakula na upungufu mkubwa wa umeme. Kwenye hali hii hatutaweza kufanya maendeleo.

Aidha, nchi yetu ilikumbwa na wimbi kubwa la wakimbizi kufuatia machafuko yaliyokuwa yanaendelea kwenye Ukanda wa Maziwa Makuu. Vilevile, kulikuwa na tatizo kubwa la UKIMWI lililoathiri ustawi wa jamii na nguvukazi ya Taifa. Utekelezaji pia ulikumbana na mdororo mkubwa wa kiuchumi wa mwaka 2008 na baadaye 2020 ukatokea mlipuko wa UVIKO-19.

Hivi sasa tunaendelea kupambana na athari za ongezeko la bei ya mafuta duniani na uhaba wa Dola za Marekani, fedha ambayo inategemewa sana duniani.

Nimeainisha changamoto zote hizo, ili tunapoandika ndoto yetu, tutambue kwamba, yapo matukio makubwa ya kidunia yanayoweza kuathiri utekelezaji wa Dira yetu. Kwa kuwa Dira inabainisha malengo na kutupa mwelekeo, lazima izingatie matukio ya dharura yanayoweza kuibuka duniani na hapa nchini. Hivyo, mjadala tunaouanza kuhusu Dira yetu inabidi utambue ukweli huo, na tujadili pia kuhusu mbinu za kujihami na kujenga uhilimivu wa jamii na uchumi, na kuwa na mfumo mzuri wa kubaini viashiria hatarishi na kisha kuweka mikakati ya kudhibiti hatari, au kupunguza makali.

***Ndugu wananchi*,** Maendeleo ya kiteknolojia duniani yanaambatana na fursa na changamoto. Kwa mfano, masuala ya akili bandia, teknolojia ya sarafu za kidijitali (*crypto currencies*) na hitajio la teknolojia ya nishati mbadala inaweza kuwa fursa au changamoto kwetu. Tukiwa na uelewa wa mambo na mipango mizuri tunaweza tukazitumia fursa hizo kwa manufaa ya nchi yetu. Kinyume chake tusipokuwa na mipango thabiti mambo hayo yataleta changamoto kwa Taifa letu. Ndio maana nilisema usipopanga kujipangia basi utapangiwa.

Mabadiliko haya sio upande wa teknolojia pekee, kwa upande wa mazingira na mabadiliko ya Tabianchi, inatarajiwa kutakuwa na ongezeko kubwa la biashara ya hewa ukaa yaani *carbon market*. Hivyo, tunatakiwa tuwe na mjadala wa kwa namna gani nchi yetu inakuwa na uwezo wa kutambua kwa haraka na kuweza kutumia fursa zitokanazo na mabadiliko ya Tabianchi.

## MISINGI *(PRINCIPLES)* YA KUZINGATIWA KWENYE MCHAKATO WA KUANDAA DIRA MPYA

***Ndugu zangu,*** Mnamo tarehe 5 Julai mwaka huu nilisaini Muswada wa Sheria ya kuanzisha Tume ya Mipango. Kifungu cha 5 (1)(a)-(c) kimeweka muundo wa Tume hiyo, ambapo Mjumbe wake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Wajumbe wengine ni Waziri mwenye dhamana ya Mipango ya Taifa, Waziri wa Fedha na Wajumbe wengine wanne, ambao sio wajumbe wa kudumu. Kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (2)(b) cha Sheria hiyo, kimeainisha moja kati ya majukumu ya Tume ya Mipango, kuwa ni kuandaa Dira ya Maendeleo ya Taifa.

Kwa hiyo, kufuatia mabadiliko haya ya sheria, suala la kuwa na Dira ya Taifa, sio tena utashi wa Rais aliyepo madarakani wakati huo, bali ni suala la kisheria. Kama ulivyoelezwa hapa mchakato wa uandishi wa Dira, kutakuwa na timu zitakazoratibu zoezi hili. Timu hizo ni, Sekretariati ya Dira, Timu Kuu ya Kitaalam ya Dira na Kamati ya Kitaifa ya Dira, kama zilivyotambulishwa hapa.

Ninafurahi kwamba, uteuzi wa Timu Kuu ya Kitaalam imeundwa kwa kuzingatia ubobezi kwenye sekta mbalimbali na uzoefu kwenye sekta binafsi na sekta za umma, lakini pia kuna vijana na taasisi za kijamii. Niwapongeze sana wanakamati hao, kwa kuaminiwa kushika nafasi hizo. Binafsi sina mashaka na weledi, uzalendo na umakini wa Timu hii. Kuna wanadiplomasia, wataalam wa sheria za uwekezaji, wataalam wa mifumo ya kompyuta, na zaidi ya yote Mwenyekiti wake ni mtaalam wa kilimo, maendeleo vijijini na uwekezaji.

Pamoja na uzoefu wao, na Hadidu za Rejea walizo nazo, nami nilidhani niwawekee misingi inayotakiwa kuzingatiwa katika zoezi la kukusanya maoni na kuanza uandaaji wa Dira ijayo. Misingi hiyo ni ifuatayo:

i. **Ushirikishwaji** wa wadau wote muhimu;
ii. Malengo au *aspirations kwenye Dira hiyo zizingatie* **uhalisia** wa ndani ya nchi na mazingira ya Dunia;

iii. Kuzingatia **mafunzo** yaliyotokana na utekelezaji wa Dira iliyopita (lessons learnt);

iv. **Mwendelezo** kwa mafanikio na masuala mazuri yaliyotokana na Dira ya sasa (*sustainability*). Yale ambayo ni mazuri yaweke mipango ili yaendelee;

v. Kuzingatia **misingi, maadili na tunu za Taifa letu**.

***Ndugu zangu***, mmeyasikia mapito ya utekelezaji wa Dira yetu na changamoto tulizokutana nazo. Inawezekana kabisa, baadhi ya changamoto zilitokana na ukweli kwamba hatukuwa na uzoefu wa mipango ya muda mrefu, kwani hii ilikuwa ni Dira yetu ya kwanza tangu tupate uhuru. Wengine wanasema ***ujinga ni wakati wa kwenda, wakati wa kurudi unakuwa umeshasoma umeshaerevuka***. Nasi kama tumekosea kwenye Dira ya kwanza, kwenye Dira ya pili tumeshapata uzoefu wa kutosha, twendeni tukajipange vizuri. Tuhakikishe changamoto zilizotokea kwenye utekelezaji wa Dira inayomalizika hazijirudii kwenye Dira mpya.

Ninapohitimisha hotuba yangu, ninaomba nisisitize na kuelekeza mambo yafuatayo;

(i) **Kwanza,** Sekretarieti za Mikoa zitoe ushirikiano na ziisaidie Tume ya Mipango kwa uratibu wa kuwafikia wananchi wengi kwenye zoezi la kukusanya maoni;

(ii) **Pili,** kila mwananchi aliyepo nchini au ughaibuni (*diaspora*) ahakikishe anashiriki kikamilifu katika uandishi wa Dira mpya, wao binafsi au kupitia makundi yao, kwa kutoa maoni kupitia njia za kisasa zitakazoainishwa na Tume ya Mipango; na

(iii) **Tatu,** baada ya kukamilisha uandishi wa Dira ijayo, Tume iandae makala fupi ya Dira hiyo ambayo itakuwa na lugha rahisi inayoeleweka kwa wananchi wengi. Kutakuwa na ripoti kubwa ya kitalaam itakayotumika na wataalam na ulimwengu, lakini twende tukawaandikia wananchi makala rahisi wanayoweza kuisoma na kuielewa.

***Ndugu Wananchi,*** Ninawashukuru tena wadau wote mliojitokeza kuhudhuria Mkutano huu wa kwanza wa kitaifa wa Dira ya Maendeleo ya Taifa. Niwatakie ushiriki mwema katika zoezi la kuandaa dira, na ***InshAllah,*** tutakutana tena katika mwendelezo wa Mikutano mingine hadi kufikia mkutano wa kuizindua Dira mpya.

Baada ya kusema maneno hayo, sasa natamka rasmi kwamba, Mchakato wa uandishi wa Dira mpya ya Taifa, 2025/2050 umezinduliwa Rasmi.

Nawatakia maadhimisho mema ya miaka 62 ya Uhuru wetu.

**Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika!**

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza !**